# KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHUO CHA VETA MAFIA KWA MWAKA WA MASOMO 2025/26

Ndugu.:

Mkuu wa Chuo Cha VETA Wilaya ya Mafia anapenda kukufahamisha kwamba umechaguliwa kujiunga na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi VETA Mafia katika fani uliochagua kama ulivyoorodheshwa.

Chuo hiki kipo mkoa wa Pwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, kilometre 13 tokea kiwanja cha Ndege Mafia na kilometer 15 kutokea Bandari ya Mafia.

**MAELEZO**

1. Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe 13/01/2025
2. Mafunzo yatachukua muda wa miaka miwili.
3. Unatakiwa kuthibitishwa na daktari wa serikali kuwa unayo afya nzuri ya kumudu mafunzo katikafani uliyochagua.
4. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa zilizoainishwa kwenye taarifa hizi.
5. Unatakiwa kununua vifaa ainishwa kwa matumizi yako chuoni.
9. Unatakiwa kuriport ndani ya wiki moja kutokea tarehe ya kufungua chuo

**MAHITAJI YA VIFAA UNAVYOTAKIWA KUJA NAVYO**

A. Mashati mawili meupe ya tetron – mikono mirefu.
B. Suruali mbili za bluu kwa wavulana au Sketi Mbili za bluu kwa wasichana (ISTEM No1). Zisiwe za kubana na zisiwe fupi (suruali isiwe juu ya vifundo(ankle) vya miguu na sketi isiwe juu ya magoti)
C. Jozi moja au mbili ya viatu vyeusi (vya ngozi vyenye kamba kwa wanaume) na soksi nyeupe pea mbili.
D. Mavazi na vifaa vya usafi binafsi. (Fagio la ndani, kwa ajili ya usafi wa chumbani)
E. Madaftari (counter book ) saba.
F. Kwa wale watakaokaa bwenini waje na shuka mbili (pinki kwa wasichana, bluu kwa wavulana),mto wa kulalia, bakuli (SIO PALSTIKI), sahani (SIO PLASTIKI), kikombe (SIO PLASTIKI), kijiko cha chakula, ndoo moja ndogo kwa ajili ya bafuni. Picha ndogo 1 (passport size), jembe kwa ajili ya usafi wa mazingira.
G. Karatasi nyeupe (photocopy paper A4 - 21cm x 29.7cm, 80 GSM) rim moja.
H. Viatu aina ya raba na tracksuit ya blue kwa ajili ya michezo.
I. Overcoat ya kaki kwa wanafunzi wa fani ya umeme, Overcoat ya blue kwa wanafunzi wa fani ya ushonaji.
J. **FAHAMU :**

i. Vitu hivi vitakaguliwa siku ya kuwasili chuoni.

*ii. Nyaraka zote hizi ni muhimu kuja nazo siku ya kuwasili chuoni zikiwa zimejazwa ipaswavy.*

Mafia DVTC, S.L.P 36, Simu: +255 743 021 726
Barua pepe: mafiadvtc@veta.go.tz

A. **Ada mwaka wa Kwanza**

| MIHULA | ADA | JUMLA | BWENI AU KUTWA |
|---|---|---|---|
| I | 60,000 | **60,000.00** | BWENI |
| | 30,000 | **30,000.00** | KUTWA |
| | | | |
| II | 60,000 | **60,000/=** | BWENI |
| | 30,000 | **30,000/=** | KUTWA |

**B: Michango**

| N | KIFAA | MALIPO |
|---|---|---|
| i | Bima ya afya (NHIF) kwa wasio na Bima | 50400.00 |
| ii | Nembo ya VETA | 5,000.00 |
| iii | Tshirt | 20,000.00 |
| iv | Kitambulisho cha mwanachuo | 10,000.00 |
| v | Serikali ya Wanafunzi (MASO) na Michezo | 15,000.00 |
| vi | Godoro | 20,000.00 |
| | | **120,400.00** |

D. **JUMLA YA ADA NA MICHANGO**

| MIHULA | WASIO NA BIMA | WENYE BIMA | BWENI AU KUTWA |
|---|---|---|---|
| I | **180,400.00** | **130,000.00** | BWENI |
| | **150,400.00** | **100,000.00** | KUTWA |
| | | | |
| II | 60,000 | **60,000/=** | BWENI |
| | 30,000 | **30,000/=** | KUTWA |

**FAHAMU:**.

Malipo ya Ada yatalipwa kwenye **control namba** itakayotolewa na muhasibu chuoni.

## SHERIA ZA CHUO CHA VETA MAFIA:

Ili kufanikisha mafunzo ya ufundi stadi kila mwanafunzi anatakiwa kufuata sheria zifuatazo:-

1. **MAHUDHURIO:**
   - (a) Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1:30 asubuhi. Hii ina maana ifikapo saa 1:30 asubuhi wanafunzi wote wawe wameshafika chuoni.
   - (b) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya chuo yoyote ile bila ya RUHUSA ya Mwalimu wa zamu na mwalimu wa darasa.
   - (c) Mwanafunzi wa kutwa (Day), au awapo nje ya chuo kwa ruhusa maalum, akiwa kapatwa matatizo au dharura yeyote na kushindwa kuhudhuria au kurudi chuoni, lazima taarifa zifike chuoni, bila ya kufanya hivyo ni kosa.
   - (d) Mahudhurio ya darasani chini ya 85% (asilimia themaninini na tano) mwanafunzi atanyimwa cheti cha kuhitimu mafunzo.
   - (e) Vyumba, Madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo viti au meza za chuo. Adhabu kali itatolewa kwa atakaefanyae hivyo.

**2.** **MAVAZI:**

(a) Sare ya chuo ni suruali (kwa wanume) au sketi (kwa wasichana) ya dark bluu na shati jeupe la mikono mirefu na T-shirt ya VETA. Sare hiyo ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo chuoni nyakati za masomo. Wakati wote shati liwe limechomekewa.

(b) Mavazi ya kubana, yasiyo ya heshima, pensi au kaputula, skirt fupi, hayaruhusiwi

(c) Ovaroli livaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.

(d) Viatu vyenye visigino virefu na kanda mbili au viatu vya wazi (sandals) kubadhi, haviruhusiwi kuvaliwa chuoni nyakati za masomo.

**3.** **USAFI WA MWILI:**

(a) Hairuhusiwi kuvaa hereni ndefu za kuning'inia, pete (isipokua ya ndoa), bangili nyingi na kwa kipindi chote cha muda wa darasani.

(b) Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kali mda wowote uwapo chuoni.

(c) NYWELE NA NDEVU KWA WAVULANA:

i. Zikatwe ziwe fupi, KIPARA hakiruhusiwi kabisa.

ii. Ndevu haziruhusiwi.

iii. Ndevu za aina zote haziruhusiwi mustachi au sharubu.

(d) NYWELE NA KUCHA KWA WASICHANA:

i. Nywele ziwe fupi au zisukwe vizuri, rangi kwenye nywele hairuhusiwi

ii. Hairuhusiwi kuwa na kucha ndefu, wala kupaka rangi za kucha

(e) MANUKATO, KUPIGA MSWAKI NA KUOGA:

i. Hairusiwi kujipulizia manukato yenye harufu kali

ii. Unatakiwa kupiga mswaki mara mbili kwa siku (usinuke mdomo)

iii. Unatakiwa kuoga kwa maji safi na sabuni walau mara moja kwa siku (usinuke jasho)

**4.** **USAFI WA MAZINGIRA**

(a) Kila mwanafunzi anatakiwa kutunza mazingira ya chuo kwa ujumla wake kwa kufanya usafi wa chumba anacholala, chooni, bwenini, mazingira ya nje pamoja nakutotupa taka ovyo na kupanda na kutunza miti.

(b) Wanafunzi wanatakiwa kutunza miti iliopo mazingira ya chuo na kupanda miti kwa ajili ya matunda na kivuli

(c) Wanafunzi wanatakiwa kutumia maji na umeme vizuri na sio kufuja. Ufujaji ni kosa.

**5.** **WIZI NA USALAMA**

(a) Vitendo vyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi ameiba mali ya chuo au mwanafunzi mwenzake, basi atafukuzwa chuo mara moja na kufikishwa kwenye vyombo vya dola.

(b) Ukipoteza kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa na ukakinunue kifaachenyewe au ulete badala ya ulichokipoteza.

(c) Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo pasi ya kukitolea taarifa na kukuandikisha.

(d) Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na getini.

(e) Mwanafunzi atatakiwa kuonyesha kitambulisho chake kwa mlinzi getini, mda wote anapoingia na kutoka chuoni

(f) Mwanafuzni atatkiwa kutoa taarifa kwa walinzi au walimu pindi aonapo tukio lolote la uhalifu au uharibifu wa mali za chuo au mwanafunzi,

(g) Wanfunzi hawaruhusiwi kuitembelewa na wageni chuoni pasi ya kuwandikisha na kuwatambulisha kwa walinzi.

(h) Watu wasio wanafunzi hawruhusiwi kulala ndani ya chuo. Wanafunzi wa kutwa watalala kwa kibali maalum toka kwa mkuu wa chuo kupitia kwa mlezi wao.

**6. UGOMVI NA MATUSI:**

Matusi, kupigana au kushambuliana ni makosa ya jinai. Atakayepatikana akijihusisha na matendo yanamna hiyo atafukuzwa chuoni na kukabidhiwa kwenye vyombo vya dola mara moja.

**7. ULEVI NA MADAWA YA KULEVYA**

i. Iwapo itabainika mwanafunzi analewa au amelewa au kunywa pombe akiwa ndani ya eneo la chuo adhabu yake ni kufukuzwa chuo.

ii. Iwapo itabainika mwanafunzi anavuta bangi au kutumia au kuuza au kushiriki katika shughuli za madawa ya kulevya atafukuzwa chuoni na kukabidhiwa kwenye vyombo vya dola mara moja.

**8. MAPENZI NA UJAUZITO.**

(a) Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au kati yake na mfanyakazi wa chuo hairuhusiwi kabisa. Kufanya hivyo kutapelekea kusimamishwa masomo au kuondolewa boarding (Bweni) au kupoteza nafasi ya masomo.

(b) Mwanafunzi wa kiume au wa kike haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi watumishi nyumba za watumishi bila ya kibali au ruhusa. Kufanya hivyo kutapelekea kusimamishwa masomo au kuondolewa boarding (Bweni) au kupoteza nafasi ya masomo.

(c) Mda wote mwanafunzi wa kiume haruhusiwi kuingia bweni la wanafunzi wa kike au mwanafunzi wa kike kuingia bweni la wanafunzi wa kiume. Adhabu kali itatolewa ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo kwa yeyote atakaekutwa na kosa hilo.

(d) Mda wowote wanafunzi wa kike na wakiume hawaruhusiwi kukaa au kuwa wawili faraga, mazungumzo au masomo yafanyike sehem za wazi zilizopangwa na chuo.

(e) Kufanya mapenzi ndani ya eneo la chuo ni MARUFUKU. adhabu yake ni kufukuzwa chuo.

(f) Wanafunzi wote wenye ujauzito wanatakiwa kutoa taarifa kwa mlezi wao na mwalim wa darasa, wanafunzi hao wanaruhusiwa kuendelea na masomo ila watashauriwa kukaa day (kutwa) ili kuepuka usumbufu.

**9. MIGOMO:**

Suala lolote la migogoro au sintofahamu lipelekewe taarifa kwa serikali ya wanafunzi na kisha uongozi wa chuo. Migomo ni marufuku, na kuchochea migomo ni kosa chuoni. Atakayeshawishi au kusababisha mgomo atafukuzwa chuoni mara moja.

**10. LUGHA YA MAWASILIANO CHUONI**

Lugha inayotumika kuendeshea masomo ni kiingereza, hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kujifunza kuongea kiingereza mda wote wawapo chuoni, adhabu itatolewa kwa yeyote asietii.

**11. DINI NA USTAARABU WAKE**

(a) Kutakua na muda au vipindi vya dini chuoni ili kuimarisha maadili

(b) Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu dini ya mwengine pasi kudhihaki hata kidogo


**12. MATUMIZI YA SIMU ZA MKONONI**

(a) Ni marufuku kuwasha simu za mkononi wakati wote wa vipindi.

(b) Ni marufuku kusambaza au kuwaonyesha picha za uchi au zisizo na maadali chuoni.

**ONGEZEKO LA SHERIA KWA WANACHUO WA BWENI**

13. Mwanachuo ataruhusiwa kutoka nje ya Chuo siku zifuatazo tu:
    i. Jumapili kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni
    ii. Jumamosi kuanzia saa 12:00 mchana hadi saa 12:00 jioni
    iii. Hairuhusiwi kutoka nje ya Chuo wakati wowote bila kibali.
14. Mwanachuo yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya eneo la Chuo anapaswa kuwa amevaa kitambulisho cha Chuo na atajiandikisha lango kuula Chuo. Mwanafunzi atakayeonekana nje ya maeneo ya Chuo bila kitambulisho atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang’anywa nafasi ya kulala bwenini au kufukuzwa chuoni.
15. Mwanachuo atakayepatikana na kosa la kulala au kuwa nje ya Chuo bila kibali atasimamishwa masomo.
16. Hairuhusiwi kupikia chakula bwenini, na atakayekiuka sheria hii atachukuliwa atafukuzwa chuo kwa kosa la ktaka kuunguza moto majengo ya chuo.
17. Kuzuia wadudu kama mende, mda wote wanafunzi watakula chakula kwenye bwalo la chakula nasio vyumbani, isipokuwa wagonjwa wenye kibali.
18. Saa nne kamili usiku, wanachuo wote wanatakiwa wawe ndani ya vyumba vyao vya kulala.
19. Mwanafunzi wa bweni atajaza kibali maalum kumruhusu kulala nje ya chuo.
20. Wageni wote wanaokuja kuwasalimia wanafunzi waje baada ya muda wa masomo au week end, mwisho wa kutembelewa ni saa 12:00 jioni.



……………………………………..

**Salim Jumbe**

**Kny: MKUU WA CHUO**

VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY
MEDICAL EXAMINATION FORM

**Date………………………**

**THE MEDICAL OFFICER**

...……………………………

………………………………

……………………………………

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION:**

Name of trainee ……………………………………………………..
Please examine the above named trainee to his/her fitness to undergo training

Eye sight…………………………………………………

Hearing………………………………………………..

Asthma……………………………………………………

Other serious diseases…………………………………........

MEDICAL CERTIFICATE:

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for training as above.

Date …………………………………….

Designation………………………………

Signature and ………………………………

official stamp…………………………………

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**a)** MWANACHUO

Mimi....................................................................
Fani ya……………………………………………
Ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa, pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo ambazo nimezisoma nakuzielewa vizuri.
Sahihi ……………………………………..Tarehe………………………….

**b)** MDHAMINI

Mimi……………………………………………………………………
ambaye(Mzazi/Mlezi/Kaka/Dada n.k) wa mtajwa hapo juu nathibitisha kuwa ninamdhamini na nitamlipia gharama zote za mafunzo ikiwa ada na michango mingine kama ilivyoelekezwa katika maelezo ya kujiunga na Chuo wakati wote wa mafunzo.

Simu……………………………………

Sahihi ………………………………

Tarehe ………………………….